

TAKWIMU ZA ULANGUZI WA WANADAMU ULIMWENGUNI KOTE



Kuna watu **milioni 50** waliofanywa watumwa ulimwenguni leo.¹



Ulanguzi wa wanadamu hutoa takribani **dola bilioni 236** za Marekani kwa mwaka.²



Takribani mwanadamu **1 kati ya 4** walioathiriwa na ulanguzi wa wanadamu ni watoto.³



Ulanguzi wa wanadamu hufanyika **katika kila eneo** ulimwenguni na unaweza kufanyika kwa mtu yeyote.

ISHARA ZA ULANGUZI WA WANADAMU

Tumia ishara hizi kutambua uwezekano wa mtu kuwa mwathiriwa wa utumwa wa kisasa.

HUDHIBITIWA NA MTU MWINGINE

Huandamana na mtu anayewadhibiti, na hawajizungumzii wenyewe, bali huzungumziwa na mtu mwingine.

MATEMBEZI YAO HUDHIBITIWA

Husafirishwa kwenda au kutoka kazini, au huishi na kufanya kazi mahali pamoja. Huonyesha ishara kwamba matembezi yanadhibitiwa.

HAWALPWI MSHAHARA

Hawawezi kujiwekea malipo yao wenyewe na hulazimishwa kumpa mtu mwingine. Katika visa vingi, huyo mtu huwa ana deni ambalo anafanya kazi ili alilipe.

HAWANA VITAMBULISHO RASMI

Hawana paspoti zao, vitambulisho, au hati halali.

WANA HOFU KUPITA KIASI, WANA

HUZUNI, NA TABIA YA UTIIFU

Wanaogopa kuongea na watu wa nje na mamlaka kwa kuwa wanafuatiliwa kwa ukaribu sana na Kudhibitiwa na walanguzi wao.

HUDANGANYWA KWA KUPEWA

AHADI ZA UONGO ZA KAZI

Kazi zao halisi ni tofauti na ile kazi waliyokubali wakati ilipotangazwa.

UKISHUKU HALI HII, PIGA RIPOTI.

Wameonyesha kuwa hawawezi kuacha hali yao wanayoishi au hali yao ya ajira.

1. Global Slavery Index. (2022). Global Slavery Index Report 2022.

2. Profits and Poverty: The Economics of Forced Labour (2024)

3. Global Slavery Index. (2022). Global Slavery Index Report 2022.

UKISHUKU HALI HII, PIGA RIPOTI.

Changanua kielektroniki alama ya siri ya QR ili uihifadhi, uisambaze, na upigie nambari hizi unaposhuhudia ishara za ulanguzi wa wanadamu.

